



## **BODI YA BIMA YA AMANA**

**KATIKA SHAURI LA FBME BANK LTD (CHINI YA UFILISI)**

**NA**

**KATIKA SHAURI LA SHERIA YA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA, 2006 (THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, 2006)**

### **TAARIFA KWA WENYE AMANA**

**TAARIFA** inatolewa kwa wenye amana wa iliyokuwa **FBME BANK LTD** kwamba, **FBME BANK LTD** imewekwa chini ya ufilisi na Benki Kuu ya Tanzania kuanzia tarehe 8 Mei, 2017 chini ya mamlaka iliyopewa na kifungu cha 61 (1) na 41 (a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, 2006 (The Banking and Financial Institutions Act, 2006) Benki Kuu imeiteua Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board –DIB) taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 37 (1) cha Sheria tajwa kuwa Mfilisi wa benki hiyo.

Kutokana na uteuzi huo, wenye amana wote wa **FBME BANK LTD** (Depositors) wanajulishwa kwamba, kwa hivi sasa Mfilisi wa benki hiyo (Deposit Insurance Board – DIB) anafanya uhakiki wa mali na madeni ya Benki hiyo na baada ya hapo atawajulisha wenye amana (depositors) taratibu zitakazotumika kuwafidia amana zao kwa mujibu wa Sheria.

Maulizo yote yaelekezwe kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB) kwa kutumia anuani iliyotajwa hapo chini;

**Mkurugenzi**

**Bodi ya Bima ya Amana**

**Jengo la Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania**

**2 Mtaa wa Mirambo**

**Ghorofa ya 7, Mnara wa Kaskazini**

**11884 DAR ES SALAAM**

**Email: DIB-INFO@bot.go.tz**

**TEL: +255 22 223 5390**

**Fax: +255 22 223 4200**

**IMETOLEWA TAREHE 12 MEI, 2017**